# MwanaHisa

CRDB BANK PLC — Toleo la Disemba, 2015

## Yaliyomo


- Benki Yafikia Malengo Ya Kibiashara ................................ 1
- Malipo ya Gawio kufanyika kupitia Akaunti za benki ....... 2
- Toleo la Hisa Stahili lakamilika kwa Mafanikio Makubwa ............................ 3
- Kukua kwa Teknolojia katika Tasnia ya Benki ni Fursa ....... 5
- Je Wajua? ............................ 6
- Wiki ya Huduma kwa Wateja (Tarehe 5 hadi tarehe 10 Oktoba 2015) katika Picha .. 7
- Kibonzo. .............................. 8



**ANUANI**
Mhariri Mwanahisa
CRDB Bank Plc
Office Accomodation scheme
Mtaa wa Azikiwe, Ghorofa ya 4
S.L.P. 268
Dar es Salaam

Simu Na: 002 - 2117442 - 7
2114237
Fax No. 022 - 2131005
Barua pepe:
investorrelations@crdbbank.com
Tovuti: www.crdbbank.com


**MAONI KUTOKA KWA MWANAHISA**

Wanahisa wanapewa fursa ya kufikisha maoni, ujumbe au mapendekezo katika jarida hili kwa kutumia anuani inayoonekana hapo juu.

# BENKI YAFIKIA MALENGO YA KIBIASHARA

Benki ya CRDB imefanikiwa kufikia malengo ya kibiashara katika viashiria muhimu vya utendaji ikiwa ni pamoja na faida, rasilimali, mtaji na amana kama ilivyoainishwa katika mkakati wa biashara wa Miaka mitano (2013 - 2017) na Mpango wa Mwaka 2015 (*Annual budget for 2015*). Kumekuwepo pia na ukuaji wa faida ikilinganishwa na mwaka uliopita na malengo ya bajeti. **Mfano:** Faida baada ya kodi imeongezeka kutoka shillingi bilioni 71.9 iliyopatikana katika kipindi cha Januari – Septemba mwaka 2014 na kufikia shilingi bilioni 103.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia arobaini na nne (44).




***Mmojawapo wa Wafanyakazi wa Benki akimlisha keki mteja ikiwa ni ishara ya kusema Ahsante Mama kwa kutumia huduma zetu!***

Pamoja na changamoto zinazoikabili sekta ya huduma za kifedha, ikiwemo kushuka kwa kasi kwa thamani ya shillingi dhidi ya dola ya marekani, Benki imefanikiwa kukuza thamani ya Mizania yake kwa ufanisi mkubwa kama inavyoashiriwa kwa vigezo vilivyoonyeshwa katika jedwali hapa chini (kwa thamani ya bilioni ):

| Viashiria vya Utendaji | Jan – Sept. 2014 (Shilingi bilioni) | Jan – Sept. 2015 (Shilingi bilioni) | Ongezeko (Kwa asilimia %) |
|---|---|---|---|
| Rasilimali | 4,160 | 5,273 | 27 |
| Amana | 3,378 | 4,022 | 19 |
| Gharama za Uendeshaji | 180 | 218.9 | 21 |
| Mtaji | 418 | 667 | 60 |
| Faida baada ya kodi | 71.9 | 103.7 | 44 |
| Rejesho kutokana na Mtaji (ROE) | 25% | 25% | |
| Rejesho kutokana na Rasilimali (ROA) | 4.2% | 3.7% | |

Mafanikio haya yametokana na jitihada za pamoja kati ya Bodi, Menejimenti, Wafanyakazi pamoja na imani kubwa waliyonayo wateja kwa huduma zinazotolewa na Benki. Ndani ya kipindi hiki Benki imetekeleza mambo makuu ya kimkakati yafuatayo:

- Kufungua vituo vya huduma kwa taasisi za serikali *"Government Service Centers."*
- Kufanya ukarabati mkubwa na kuboresha mfumo wa kutoa huduma katika mashine za kutoa na kuweka fedha (ATMs).
- Kupanua mtandao wa Benki kwa kuongeza idadi ya mawakala na watoa huduma.
- Kuongeza Mtaji kwa kutekeleza toleo la Hisa Stahili ambapo jumla ya shillingi billioni 152 zilikusanywa.
- Kuongeza ufanisi wa mifumo ya TEHAMA ili kuboresha upatikanaji wa huduma za kibenki kupitia simu ya kiganjani (*Simbanking*).

Benki inaendelea kukabiliana na changamoto kadhaa zinazoikabili sekta ya huduma za kifedha hapa nchini kama vile: kushuka kwa thamani ya shillingi, ushindani kutoka kwa taasisi zisizokuwa mabenki katika utoaji wa bidhaa za kibenki kama vile makampuni ya simu, pamoja na mabadiliko ya masharti ya udhibiti wa shughuli za kibenki. Kwa kuendelea kutekeleza kwa kasi mkakati wa biashara wa miaka mitano (ambao umethibitika kuwa na ufanisi mkubwa), Benki inatarajia kupata matokeo bora zaidi ifikapo mwishoni mwa mwaka huu na hivyo kuwa na matarajio ya kuongeza gawio kwa Wanahisa.

## Malipo ya Gawio kufanyika kupitia Akaunti za benki

**Ili kutekeleza matakwa ya soko la hisa la Dar es salaam, Bodi ya Wakurugenzi inapenda kuwataarifu Wanahisa wote kwamba, malipo ya gawio yatafanyika kupitia akaunti ya Benki ya Mwanahisa husika kuanzia Januari 2016.**

**Mojawapo ya sababu za maamuzi haya ni kuboresha malipo ya gawio kwa Wanahisa. Hii ni kutokana na changamoto zinazojitokeza pale malipo yanapofanyika kwa hundi na kutumwa kwa njia ya Posta au simu za kiganjani. Matumizi ya njia hizi yanasababisha malipo ya gawio kuchelewa kufika kwa Mwanahisa. Ni wazi kuwa, malipo kupitia akaunti ya Benki ya Mwanahisa itaondoa usumbufu wowote unaosababishwa na malipo kuchelewa, kwani Mwanahisa atakuwa na uwezo wa kufuatilia na kuona malipo yake mara moja.**

**Bodi na Menejimenti ya Benki wanaomba kila Mwanahisa kufungua akaunti ya Benki na kuwasilisha taarifa zifuatazo kwa Katibu wa Benki kabla ya tarehe 30 Disemba 2015.**

- **Namba ya akaunti, jina la Benki na tawi.**
- **Anuani ya barua pepe.**
- **Namba ya simu ya kiganjani.**

**Benki inahitaji namba ya simu na anuani ya barua pepe ili kuweza kutoa taarifa kwa Mwanahisa mara tu malipo yanapofanyika.**

# Toleo la Hisa Stahili lakamilika kwa Mafanikio Makubwa

Hivi karibuni Benki imekamilisha rasmi toleo la Hisa Stahili ambapo imefanikiwa kufikia malengo yaliyokusudiwa. Akitangaza rasmi matokeo ya toleo la Hisa Stahili Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya CRDB aliwashukuru wadau wote wakiwemo Wafanyakazi, Wanahisa, mawakala wa soko la hisa la Dar es Salaam, mamlaka mbalimbali za usimamizi pamoja na washauri kwa kushiriki kikamilifu tangu mwanzo hadi mwisho wa toleo. Katika toleo hili jumla ya hisa mpya 435,306,424 zilitolewa na kuuzwa kwa bei ya shillingi 350/= kwa kila hisa iliyomilikiwa na Mwanahisa aliyekuwemo kwenye Daftari la Wanahisa tarehe 18 Juni, 2015 kwa uwiano wa hisa moja kwa kila hisa tano (5) zinazomilikiwa.

## Malengo ya Hisa Stahili

Lengo lilikuwa ni kukusanya shillingi billioni 152.3 ili kuiwezesha Benki kuendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Biashara wa Miaka Mitano (2013 – 2017).

## Upekee wa Toleo Hili

Akifafanua matokeo ya toleo hili la Hisa Stahili, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Dkt. Charles Kimei alisema, “toleo hili ni la kipekee kabisa kuwahi kutekelezwa katika sekta ya huduma za kifedha hapa nchini na yamkini katika kanda ya Afrika Mashariki na Kati”. Tofauti na toleo la kawaida, toleo hili lilidhaminiwa na mashirika matatu ya kimataifa yaani; International Finance Corporation (IFC), Africa Capitalisation Fund Ltd (AfCap) na CDC Group Plc  ambao kwa pamoja  walibeba jukumu la kununua hisa ambazo hazitachukuliwa na Wanahisa. Tofauti nyingine ni kwamba Wanahisa walilipwa shilingi thelathini na mbili (32/=) kwa kila hisa ambayo walishindwa kuchukua.

## Matokeo ya Toleo la Hisa Stahili

Matokeo ya toleo la Hisa Stahili ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapa chini:

| Kipengele | Idadi Ya Hisa | Thamani Kwa Shillingi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Hisa zilizotolewa | 435,306,424 | 152,357,248,400 | 100% |
| Jumla ya Hisa zilizonunuliwa na Wanahisa | 306,833,746 | 107,391,811,100 | 70% |
| Hisa ambazo hazikuchukuliwa | 128,472,678 | 44,965,437,300 | 30% |

## Malipo ya Hisa Stahili

Kama inavyoonekana katika Jedwali hapo juu idadi ya hisa ambazo hazikuchukuliwa na Wanahisa ilikuwa 128,472,678, ambazo zimenunuliwa na mwekezaji mdhamini (*underwriter)* kwa bei ya shillingi 382/= kwa kila hisa. Tofauti kati ya bei ya Mwanahisa na bei ya mdhamini ambayo ni shillingi 32/= alilipwa Mwanahisa kwa kila hisa ambayo hakuchukua. Malipo hayo yalifanyika **tarehe 17 Agosti, 2015.**

## Kuorodhesha Hisa Stahili

Benki imefanikiwa kukamilisha zoezi la kuorodhesha Hisa Stahili katika soko la hisa la Dar es Salaam tangu **tarehe 19 Agosti, 2015** kwa bei ya shillingi 400/= kwa kila hisa. Hisa mpya zilizoorodheshwa zina hadhi sawa na hisa zilizokuwepo kabla ya toleo la Hisa Stahili. Hii ni pamoja na haki ya kupata gawio pamoja na stahili zozote zitakazotangazwa, kufanyika au kulipwa kutokana na umiliki wa hisa za kawaida kwa mwaka unaoishia tarehe **31 Disemba, 2015**.

## Mafanikio Yaliyopatikana

Pamoja na changamoto chache zilizojitokeza, toleo la Hisa Stahili limetekelezwa kwa mafanikio makubwa. Benki imefanikiwa kutekeleza shughuli zote kama zilivyopangwa na kupata jumla ya makusanyo ya shillingi bilioni 152.3 ambayo ni asilimia mia moja ya lengo. Mafanikio mengine ni idadi kubwa ya Wanahisa (wapatao asilimia 70 ya Wanahisa wote) waliojitokeza kununua Hisa Stahili.

## Mabadiliko Katika Mfumo wa Umiliki wa hisa za Benki ya CRDB

Baada ya mashirika ya CDC Group Plc/International Finance Corporation/ Africa Capitalizaion Fund kukamilisha kununua hisa ambazo hazikuchukuliwa na Wanahisa, watakuwa miongoni mwa Wanahisa waliomo katika kundi la wanahisa wanaomiliki kati ya asilimia moja hadi kumi ya hisa zote za Benki. Toleo la Hisa Stahili, limeongeza idadi ya hisa za Benki hadi kufikia bilioni 2.6. Idadi ya hisa kwa makundi mbalimbali ya Wanahisa ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

| Jina/Kundi la Wanahisa | Idadi ya Hisa | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| **Juu ya asilimia Kumi (*Above 10%*)** | | |
| DANIDA Investment Fund | 548,067,648 | 21.0 |
| Parastatal Pension Fund (PPF) | 260,882,095 | 10.0 |
| **JUMLA** | **808,949,743** | **31.0** |
| **Kati ya asilimia Moja hadi Kumi (*Above 1% and less than 10%*)** | | |
| CDC Group Plc/International Finance Corporation/Africa Capitalization Fund Ltd | 130,652,858 | 5.0 |
| Pinebridge | 106,065,500 | 4.1 |
| Aunali Rajabali and Sajjad F. Rajabali | 91,616,675 | 3.5 |
| Blakeney Investors | 82,711,549 | 3.2 |
| General Partners IV Ltd | 66,098,870 | 2.5 |
| LAPF Pension Fund | 58,077,549 | 2.2 |
| PSPF Pension Fund | 37,837,620 | 1.4 |
| Hans Aingaya Macha | 32,764,200 | 1.3 |
| National Health Insurance Fund (NHIF) | 32,040,040 | 1.2 |
| Western Zone Tobacco Growers Cooperative Union Ltd | 30,000,000 | 1.1 |
| CMG Investment Limited | 29,330,971 | 1.1 |
| Altree Custody Services | 25,204,869 | 1.0 |
| **JUMLA** | **722,400,701** | **27.6** |
| **Chini ya asilimia Moja (*Below 1%*)** | | |
| WANAHISA ZAIDI YA 28,000 | 1,080,488,140 | **41.4** |
| **JUMLA YA MTAJI ULIOLIPWA** | **2,611,838,584** | **100.0** |

# Kukua kwa Teknolojia katika Tasnia ya Benki ni Fursa - Sehemu ya pili

Katika jarida la Mwanahisa toleo lililopita, tulitoa utangulizi wa makala hii. Ambapo tulieleza maana halisi ya teknolojia katika tasnia ya benki na kueleza kwa ufupi mapinduzi yanayoletwa na kukua kwa teknolojia. Katika jarida hili (kama tulivyoahidi) tumeainisha baadhi ya fursa zinazotokana na kukua kwa teknolojia katika tasnia ya benki.

Kwa ufupi teknolojia katika tasnia ya benki inajumuisha vifaa na aina zote za mifumo inayoiwezesha Benki kuwasiliana, kusambaza, kutunza, kutangaza na kubadilishana taarifa na kutoa huduma. Hii inajumuisha vitendea kazi kama redio, luninga, simu, *satellite dishes*, tarakilishi/*computer*, pamoja na mtandao mzima wa mawasiliano.

**Fursa kutokana na Ukuaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

Maendeleo kwenye teknolojia ya mawasiliano, yameibua fursa lukuki kwa Benki ya CRDB na wadau wake wote kwa ujumla. Maendeleo haya yameiwezesha Benki kuunganisha matawi yake yote nchini na kufanya kazi kama tawi moja kubwa. Teknolojia inaleta raha sana, pale unapoona mteja mathalani kutoka Arusha anapata huduma kwenye matawi hapa Dar es Salaam, au kwa Wakala, kama vile yupo katika tawi alilofungulia akaunti. Ni wazi kuwa, hali hii isingewezekana pasipo matumizi ya TEHAMA.

Maajabu mengine tunayoyaona, ni pale ambapo mteja wa benki nyingine anaweza kupata huduma za kibenki kupitia mtandao wa benki ya CRDB. Huduma hii, imepunguza sana gharama za uendeshaji wa Benki na kurahisisha huduma kwa wateja. Kwa kutumia kadi ya ATM, mteja wa benki anaweza kupata huduma kutoka ATM ya benki yoyote, kwa wakati wowote.

Vilevile, ukuaji wa teknolojia ya mawasiliano, unaiwezesha Benki kuunganisha matawi, mawakala, mashine za kutolea fedha (*ATMs*), vifaa vya huduma vya POS na simu za kiganjani, vyote kwa pamoja,




*Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Plc, Dkt. Charles S. Kimei pamoja na Mkurugenzi wa Maxcom Afrika Bw. Juma Rajabu wakisaini Mkataba wa Makubaliano ya Kibiashara ambapo kampuni ya Maxcom imekuwa Wakala mkubwa wa Fahari Huduma kupitia vituo vya MaxMalipo. Mkataba huu ni moja ya kielelezo cha matumizi chanya ya fursa zinazotokana na maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.*

kwenye mfumo mmoja wa Benki. Hii inampunguzia mteja gharama, muda na usumbufu wa kutembelea tawi la Benki, pale anapohitaji huduma. Kwa sasa, huduma zote za kibenki zinaweza kupatikana kupitia simu ya kiganjani (*Simbanking*), mtandao wa *internet* (*internet banking*) na kwa kupitia mawakala wa Fahari Huduma walioko nchi nzima.

Kupitia kwa Wakala wa Fahari Huduma (ambao idadi yao ilifikia 1,769 mwishoni mwa mwezi Septemba 2015) wateja wanaweza kufanya miamala yote ya kibenki, pamoja na kufungua akaunti ndani ya dakika kumi, kupokea na kulipa fedha, kufanya malipo ya ankara pia kupokea marejesho ya mikopo waliyopewa na Benki ya CRDB.

Fursa nyingine inayotokana na ukuaji wa teknolojia ya mawasilianno ni wateja kuwezeshwa kununua au kulipia bidhaa na huduma kupitia mitandao (*online purchase*), na kutekeleza miamala ya malipo ya Ankara (*bills payment*) kupitia moja ya njia za mitandao. Njia hii inatoa fursa za kibiashara kwa watanzania walio wengi, na kuipatia Benki kipato kutokana na huduma hii.

Kama ilivyo katika usemi kuwa, 'maendeleo ya teknolojia yamefanya dunia kuwa kijiji", kadhalika kwa tasnia ya kibenki, kwani wateja nchi nzima wameunganishwa na Benki, ambapo wanaweza kupata huduma mahali popote, masaa 24 na kwa urahisi.

Ijapokuwa, wananchi walio wengi bado wako nje ya mtandao rasmi wa kibenki (*financially excluded*) na hawana uwezo wa kufungua akaunti, kupitia mifumo inayowezeshwa na teknolojia ya mawasiliano, wananchi walio wengi wanaendelea kufikishiwa huduma za Benki ya CRDB.



# Je Wajua?

Kuanzia mwaka huu wawekezaji walioko ndani na nje ya nchi ya Tanzania wanaweza kufanya biashara ya hisa kupitia simu ya kiganjani?

Soko la Hisa la Dar es Salaam hivi karibuni lilizindua rasmi biashara ya hisa kupitia simu za kiganjani. Uzinduzi huo ulifanyika tarehe 19 Agosti, 2015. Lengo kuu ni kuwezesha Soko la Hisa kuwafikia wawekezaji walio wengi zaidi, ndani na nje ya nchi ili kupanua ushiriki wao na kuboresha hali ya ukwasi katika masoko ya kifedha. Hii ni fursa muhimu inayomuwezesha mwekezaji kupanua ushiriki wake katika soko la hisa na kuharakisha maendeleo ya kiuchumi kwa taasisi na wawekezaji binafsi. Hii ni kutokana na ukweli kuwa huduma hii inamuwezesha mwekezaji kufanya biashara ya hisa wakati wowote, mahali popote ndani ya muda wa kazi, na kwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizowekwa na soko la Hisa la Dar es Salaam.
Hadi sasa huduma hii imewavutia watu wengi, kwani zaidi ya wawekezaji elfu moja wameshajiunga. Ndani ya kipindi cha miezi miwili baada ya kuzinduliwa rasmi, zaidi ya miamala elfu mbili ilikwisha kufanyika na mapato zaidi ya shillingi millioni sitini yamepatikana hadi sasa.

***Huduma hii inamuwezesha mwekezaji kufanya yafuatayo*:**

- **Kusajili wawekezaji wapya kupitia Simu ya Kiganjani**

Mwekezaji anachotakiwa kufanya ni kubofya *150*36# kwenye simu yake ya Kiganjani ili kuanza zoezi la usajili. Baada ya hapo simu itamtaka kujaza jina lake la kwanza, la kati na jina la ukoo, kisha atajaza sanduku la Posta pamoja na mkoa anakoishi. Mwekezaji atatakiwa kuchagua aina ya kitambulisho anachotumia na kujaza namba ya kitambulisho hicho. Baada ya kuthibitisha taarifa zake na kuwasilisha maombi yake, mwekezaji atapokea namba ya siri ambayo atatakiwa kuitumia kila mara atakapokuwa anahitaji kununua hisa kwa kubofya *150*36# kwenye simu yake ya kiganjani.

Mwekezaji aliyepo atatakiwa kuingiza namba ya hati yake ya Hisa yaani "CDS account number". Hii ni namba maalum inayo mtambulisha mwekezaji ambayo huandikwa kwenye cheti chake pale anaponunua hisa. Baada ya mwekezaji kuingiza namba hii (kutokana na maelekezo aliyopata kutoka kwenye simu yake ya kiganjani) atatakiwa kuchagua wakala (kutoka kwenye orodha ya mawakala itakayoonyeshwa) anayependa kufanya naye biashara. Baada ya kuwasilisha jina la wakala

anayependa kufanya naye biashara, atasubiri uthibitisho kutoka kwa wakala husika kabla ya kuanza biashara yoyote. Baada ya kupokea uthibitisho kutoka kwa wakala husika, ndipo mwekezaji atapokea namba ya siri, ambayo ataitumia katika kununua au kuuza hisa kwa kubofya *150*36# kwenye simu yake ya kiganjani.

- **Kununua na kuuza hisa pamoja na kuangalia dhamana halisi ambazo mwekezaji anamiliki dhidi ya dhamana zinazoonekana kwenye akaunti binafsi ya mwekezaji.**

Baada ya kusajiliwa, mwekezaji atapokea namba ya siri ambayo ataitumia kufanya biashara ya hisa wakati wowote, kwa kutumia simu yake ya kiganjani. Hata hivyo, biashara ya hisa kupitia simu za kiganjani ni lazima ifanyike kwa mujibu wa kanuni na taratibu za soko la hisa, na miamala inaweza kufanyika kwenye mtandao wa soko la Hisa la Dar es salaam ndani ya saa za kazi (kuanzia saa nne asubuhi hadi saa tisa alasiri).

Mwekezaji anayetaka kununua hisa atabofya *150*36# kutoka kwenye simu yake ya kiganjani, kisha atachagua hisa anazotaka kununua. Kulingana na sheria za biashara ya dhamana, ni lazima ununuzi au uuzaji wowote wa hisa ufanyike kupitia kwa wakala aliyeteuliwa na mwekezaji. Kwa maana hiyo, wakati wowote mwekezaji anapotaka kufanya biashara ya hisa ni lazima achague wakala (kutoka kwenye orodha ya mawakala) anayependa kufanya naye biashara. Baada ya hapo mwekezaji atatakiwa kuthibitisha oda yake ndipo muamala ukamilike. Mara tu mwekezaji anapokamilisha zoezi la kununua hisa, atapokea ujumbe utakaomjulisha namba yake rejea ya malipo pamoja na maelekezo ya jinsi ya kulipia oda yake. Mara tu malipo yanapofanyika, mtandao wa huduma ya biashara ya hisa kupitia simu ya kiganjani utaipeleka oda ya mwekezaji kwenye mtandao wa soko la Hisa la Dar es Salaam.

- Kuuza Hisa na kuangalia salio. Mwekezaji anachotakiwa kufanya ni kubofya *150*36# katika simu yake ya kiganjani na kufuata orodha ya maelekezo ili kuuza au kuangalia salio la dhamana anazomiliki.


## Wiki ya Huduma kwa Wateja (Tarehe 5 hadi tarehe 10 Oktoba 2015) katika Picha



*Naibu Mkurugenzi Mtendaji Huduma Mtambuka Bi. Esther K. Kitoka akiwa amemtembelea ofisini kwake Mkurugenzi Mtendaji wa Makampuni ya ASAS iliyoko mjini Iringa Bw. Huwel Asas ili kumshukuru kwa kutumia huduma za kifedha za CRDB Bank Plc.*




*Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Dkt. Charles S. Kimei pamoja na Naibu Mkurugenzi Mtendaji Uendeshaji na Huduma Kwa Wateja Bw. Saugata Bandyopadhyay (wa kwanza kulia) wakikabidhi vifaa tiba pamoja na madawa vyenye thamani ya shillingi Millioni 20, kwa Manispaa ya Kinondoni, ikiwa ni mchango wa Benki katika mapambano dhidi ya mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu.*



*Mmojawapo wa Wafanyakazi wa Benki akihudumia wateja katika Wiki ya Huduma kwa Wateja. Wiki ya Huduma kwa Wateja hutumika pia kupokea maoni mbalimbali kutoka kwa wateja.*




*Wafanyakazi wa Benki Tawi la Nyerere, Jijini Mwanza walipotembelea kituo cha afya cha Mama wa Mungu*



CRDB BANK
The Bank that Listens

# Kibonzo






CRDB BANK
The Bank that Listens